

Ni Nini Kimekosekana Katika Picha Hii?

Soma 2 Wafalme 5:1, 9-16, 20-27. Kisha utazame picha. Ni vitu gani vimekosekana? Andika majibu yako kwenye mistari iliyo hapa chini. Uganisha nukta zilizopo ili ukamilishe picha hii, kisha uipake rangi.

- 1.....
- 2.....
- 3.....

ZUNGUMZENI PAMOJA: Gehazi alisema mambo gani mawili ya uwongo? **DOKEZO:** Soma 2 Wafalme 5:22, 25. Ni nani aliyejua kwamba Gehazi alikuwa akisema uwongo? **DOKEZO:** Soma 2 Wafalme 5:25, 26; 2 Mambao ya Nyakati 16:9; Waebrania 4:13. Kwa nini unapaswa kuepuka kusema uwongo? **DOKEZO:** Soma Methali 12:22; Yohana 8:44.

UTENDAJI WA FAMILIA: Someni simulizi hilo la Biblia pamoja. Ikiwezekana, mmoja asome sehemu ya msimuliaji, wa pili asome sehemu ya Elisha, wa tatu asome sehemu ya Naamani na watumishi wake, na wanne asome sehemu ya Gehazi.

